# FORM FOUR CLUSTER KCSE MODEL 2

# KISWAHILI PAPER 1 ANSWER

1. a) Hii ni insha ya tawasifu

b) Mtahiniwa aandike ujumbe kujihusu yeye binafsi na wala si mtu mwingine.

c) Mtahiniwa aandike katika nafsi ya kwanza na masimulizi yawe ya moja kwa moja..

d) Sura
i. Kichwa - kiandikwe kwa herufi kubwa na kupigiwa mstari

ii. Aandike majina hapa pamoja na tarehe.

e) Utangulizi Atoe maelezo mafupi kujihusu

f) Hoja muhimu

- Aeleze alikozaliwa na mwaka wa kuzaliwa
- Mahali alikozaliwa
- Wazazi wake
- Jinsia yake
- Ni mtoto wa ngapi katika familia yake.
- Kiwango chake cha elimu pamoja na vyeti na tuzo alizopata yaani:

-Shule ya msingi.

-Shule ya sekondari

- Taasisi ya kitaaluma au chuo kikuu, ataje alichosomea na alivyofaulu.

- Taaluma , kazi na tajriba
- Kazi anayofanya wakati huu pamoja na cheo au wajibu waku kazini.
- Juhudi zake maishani- amejihusisha na shughuli zipi na amefaulu vipi kaitka shughuli hizo na mchango wake katika jamii. · Vipaji vyake vingine.
- Semina/makongamano ambayo amewahi kuhudhuria.
- Anatetea nini zaidi katika jamii.

**g) Hitimisho**
Matarajio yake/azma yake/manifesto yake katika wadhifa wake mpya wa kadeti katika jeshi.

**Tanbihi**
(i) Mtahiniwa aeleze sifa zake nzuri, matendo au mafanikio yanaweza kuwa kielelezo katika jamii.

(ii) Asieleze siku yake ya kufa kwani tawasifu huandikwa na mtu aliye hai.
**(iii)**Mtahiniwa akiandika kuhusu mtu mwingine na wala si yeye binafsi atakuwa amepotoka hivyo awekwe katika kiwango cha **D.**
(iv) Insha isipochukua sura ya tawasifu aondolewe alama 4S (Sura) baada ya kusahihisha na kuiweka katika kiwango chake. 2

**2. Sababu za ukosefu wa usalama.**

- Utepetevu wa vikosi vya usalama kazini km.polisi kutowajibika. ufisadi wa askari- polisi nchini.
- Kuwapo kwa makundi haramu k.v sungusungu,mungiki.

- Ukosefu wa ujira miongoni wananchi
- Makundi ya kujitolea mhanga/imani potovu k.v Al-shabaab
- Tofauti za imani baina ya dini.
- Tofauti za vyama katika chaguzi za kila mara.
- Hisia za ukabila nchini.
- Umaskini ambao husababisha wizi/unyang'anyi.
- Matumizi ya dawa za kulenya miongoni mwa jamii za kisasa.
- Umilikaji wa silaha haramu/kinyume na sheria.
- Mila potovu k.v wizi wa mifugo miongoni mwa jamii fulani.
- Teknolojia mpya ya simu,filamu na mtandao wa wavuti km vijana huiga wayaonayo katika filamu.

**Baadhi ya suluhu**

- Kuongeza vikosi vya walinda usalama.
- Kuanzisha miradi ya vijana
- Kuimarisha ulinzi mipakani
- Kuongeza nafasi za ajira
- Suala la ufisadi kushughulikiwa na wanaohusika kuchukuliwa hatua za kisheria.
- Viongozi kujiepusha na matamshi yanayowatenganisha wananchi kwa misingi ya kikabila.
- Kuimarisha miundo msingi nchini.

3. (i) Hii ni insha ya methali

(ii) Mtahiniwa atoe kisa au visa viwili kuthibitisha maana ya methali

(iii) Mtahiniwa ashughulikie pande zote mbili za methali- Pawe na jambo kasha aonyeshe mwisho wake.

(iv) Si lazime aandike maana ya methali. Aweza kuandika kisa moja kwa moja. Maana ya methali: Kila jambo lazima liwe na mwisho wake. Matumizi: Methali hii hutumiwa kumfariji na kumliwaza mtu ambaye amepatwa na dhiki na matatizo fulani kwamba avumilie kwa kuwa matatizo hayo yatamalizika

4. a) Hii ni insha ya mdokezo.

b)Sharti mtahiniwa ajihusishe na azingatie uhusiano wa nafsi ya kwanza umoja.

c)Mtahiniwa atoe kisa kinachoafikiana na kifungu alichopewa.

d) Mtahiniwa azungumzie majanga ya kitaifa kama shambulizi la kigaidi, uvamizi, ajali n.k

**Tanbihi**

a) Mtahiniwa asipojihusisha, amejitungia swali awekwe kiwango cha D-

b) Akitoa kisa ambacho hakifikiani na kifungu amepotoka, awekwe kiwango cha D-bakishishi

c) Asipokamilisha insha kwa kifungu alichopewa atakuwa amejitungia swali.

d) Atakaye ongeongeza maneno mawili katika kifungu aondolewe ala 2z (ziada baada ya kusahihisha insha kuiweka katika kiwango chake.